

## **LEARNING BY EAR 2012**

### **“The Lost Kid – the Story of Single Mothers in Africa”**

#### **EPISODE 1: “Sleepwalkers”**

**AUTHOR: Mantegaftot Sileshi Siyoum**

**EDITOR: Stefanie Duckstein, Adrian Kriesch**

**PROOFREADER: Kate Hairsine**

**List of characters by scene:**

#### **SCENE ONE: MIDNIGHT AT BELETU’S HOUSE**

- **Begidu (m, 7)**
- **Kassech (f, 22)**
- **Narrator (m, around 35)**

#### **SCENE TWO: MIDNIGHT AT ASKALE’S HOUSE**

- **Samy (m, 6)**
- **Askale (f,21)**
- **Narrator (m, around 35)**

#### **SCENE THREE: MIDNIGHT IN JONAS’ PLACE**

- **Drunkard Minabu (m, 55)**
- **Narrator (m, around 35)**

#### **SCENE FOUR: MIDNIGHT AT BELETU’S HOUSE**

- **Papa Telahun (m, 76)**
- **Mama Beletu (f, 65)**
- **Drunkard Minabu (m, 55)**
- **Narrator (m, around 35)**

### **SCENE FIVE: MIDNIGHT IN JONAS' PLACE**

- **Kassech (f, 22)**
- **Jonas (m, 15)**
- **Narrator (m, around 35)**

### **INTRO:**

Hamjambo! Hiki ni kipindi chetu kipya cha mfululizo wa Noa Bongo Jenga Maisha Yako cha mchezo wa redio kiitwacho “ MWANA MPOTEVU- KISA CHA KINA MAMA WANAOWALEA WATOTO WAO BILA BABA ZAO BARANI AFRIKA”. Vipindi kumi vifuatavyo vinalenga maisha ya awali ya mtoto na kina mama wanaolea watoto peke yao bila baba. Hadithi hii inawahimiza kina mama hao kuwasaidia watoto wao wachanga kukua kimwili na kiakili. Twende sasa kwenye kitongoji karibu na jiji ambapo kisa hiki kinatukia. Utakutana na mvulana Begidu mwenye umri wa miaka saba anayeishi na mama yake Kassech mwenye umri wa miaka ishirini na miwili, pamoja na Jonah (ndugu mdogo wa Kassech). Rafiki ya Begidu aitwaye Samy anaishi pamoja na mamake Askale nyumba iliyo jirani. Kina mama hao wawili wasio na waume hawana elimu ya kutosha. Kassech anauza makaa ilhali Askale huuza chakula. Tusikilize sehemu ya kwanza inayohusu “WANAOTA NDOTO ZA KUWEWESEKA”. Mtoto apiga kelele ghafla kwa hofu usiku wa manane.

### **SCENE ONE: MIDNIGHT AT BELETU’S HOUSE**

1. **SFX:**                                **THUNDER AND BOLT FROM OUTSIDE**
  
2. **Begidu:**                             **(Shouts loudly, frightened).**
  
3. **Kassech:**                            Kwa nini kuniamsha usiku wa manane?  
Mpumbavu mkubwa wewe! **(Slaps)**
  
4. **Begidu:**                             Mama, ametoweka. Ametoweka! **(He cries).**

- 5. Kassech:** Nini...?
- 6. Begidu:** Mlango uko wazi.... Mama, !
- 7. Kassech:** Mungu wangu! Mlango kweli uko wazi.  
Usiondoke kwenye godoro! Kurunzi iko wapi?
- 8. SFX:** **TORCH FALLS DOWN**
- 9. Kassech:** Balaa! Glopu imevunjika.
- 10. Begidu:** Mama!
- 11. Kassech:** Nimekwambia ufunge mdomo! Tulia hapo ulipo! Liko wapi gazeti nililoleta kutoka kwenye duka la mikate?
- 12. ?**
- 13. Begidu:** Nilitumia baadhi ya karatasi zake kwenda haja.
- 14. Kassech:** Mjinga mkubwa! Sasa wataraji nione vipi gizani?
- 15. SFX:** **SCRUMPLING NEWSPAPER**
- 16. Kassech:** Haya, Hiki hapa kibiriti na gazeti lililobaki.
- 17. SFX:** **SPARKING MATCH AND FIRING  
NEWSPAPER**

**18. Kassech:** Usiondoke hapo ulipo! (**Walks fast towards the door and opens it completely**).

**19. SFX:** **NIGHT AMBIENCES AND THUNDER BECOME LOUDER**

**20. Kassech:** (**Outside**) Wewe! Simama! Simama!

**21. Begidu:** Mama! (**He cries**).

**22. NARRATOR:**

Kassech anamfuata haraka kijana fulani ambaye amemuona akitembea karibu na mlango wa nyumba yake. Lakini huyu kijana ni nani? Je ni yeye aliyefungua mlango usiku wa manane? Tutatagundua hivi karibuni, lakini Hebu sasa tuungane na Samy mwenye umri wa miaka sita pamoja na mamake Askale wanaoishi nyumba iliyoko jirani.

**SCENE TWO: MIDNIGHT AT ASKALE'S HOUSE**

**23. SFX:** **THUNDER AND BOLT OUTSIDE**

**24. Samy:** Mama, mbona Begidu amelia? Kwani anataka kunywa maji kama mimi?

**25. Askale:** Sidhani hivyo, mwanangu.

**26. SFX:** **WATER BEING POURED INTO GLASSES**

**27. Askale:** Hii hapa glasi ya maji, kunywa maji kisha ulale mwanangu.

**28. Samy:** Mama, Begidu aliniambia kwa nini anapenda kulia kila mara.

**29. Askale:** Alikwambia nini, Samy?

**30. Samy:** Aliniambia hajawahi kumuona baba yake. Kwani babake alifariki dunia?

**31. Askale:** Kunywa maji, Samy.

**32. Samy:** **(Drinks)** Lakini mama mimi sili kama Begidu.

**33. Askale:** Wewe ni mtoto mzuri! Usifanye hivyo...

**34. Samy:** Mimi pia sijawahi kumuona baba yangu.

**35. Askale:** Sasa lala mwanangu. Tayari ni usiku wa manane.

**36. SFX: SWITCHING LIGHT OFF**

**37. Askale:** Lala salama, mwanangu! **(She kisses him on his cheek).**

**38. NARRATOR:**

Kassech na Askale walikuwa wasichana wadogo wanafunzi wa shule waliopogundua kwamba walikuwa waja wazito. Kassech na Askale

sasa wanahangaikia maisha yao kila siku. Hili ni jambo la kawaida katika nchi nyingi barani Afrika. Katika Afrika Magharibi, takwimu zinaonyesha kwamba msichana mmoja miongoni mwa kila wasichana watatu huwa ameshazaa kabla ya kufikia umri wa miaka 19.

**39. SFX: WIND BLOWS**

**40. NARRATOR:**

Kitongojini, upepo mkali unazidi kupiga huku radi ikiendelea kupiga. Kassech anaondoka nyumbani kwake bila kuwaona wavulana wawili wanaojificha gizani na wanaomtazama kwa mbali. Ghafla, jirani mwingi anayelitwa Minabu anapepesuka barabarani- ni mlevi kama ilivyo kawaida yake wakati huu wa usiku.

**SCENE THREE: MIDNIGHT IN JONAS' SUBURB**

**41. SFX: WIND BLOWS AND THUNDER**

**42. SFX: DOG BARKS AT THE DRUNKARD MINABU**

**43. Minabu:** Mbwa ... unataka kuniama? Ebu njoo...  
Jaribu, ha ha ha... Kwani hujui kwamba mimi ndiye mfalme wa pekee kwenye kiza hiki!

**44. SFX: DOG APPROACHES, BARKING**

**45. SFX:                                 SOMEONE WHITSLING FROM A DISTANCE**

**46. Minabu:**                         Nyinyi! Nyinyi wawili hapo! ... Mnapanga njama gani hapo gizani? Mnataka kunitatiza usiku? Ha, Usiku ni wangu mimi! Mtaniweza? Ha ha ha...!

**47. SFX:                                 SOMEONE WHISTLING AGAIN**

**48. SFX:                                 THE DOG BARKS AND RUNS AWAY**

**49. SFX:                                 TWO PERSONS' FOOTSTEPS, RUN AWAY**

**50. Minabu:**                         Nyinyi! Nyinyi wawili hapo! Nimeshawaona! Rudini! Ha ha ha! Nimeshawaambia ...usiku ni wangu...! Mimi pweke ...wangu! Ha ha ha...!  
**(This scene blends with Minabu's voice.)**

**51. Narration:**

Naam, kina nani hao wavulana wawili waliokimbia pamoja na mbwa wao? Walikuwa wakifanya nini nje usiku wa manane? Je walikuwa na nia ya kuiba vitu katika eneo hilo? Utajua hivi karibuni. Wakati huo huo, Papa Tilahun na Mama Beletu wanachungulia kupitia dirisha dogo ili wapate kuona yanayotendeka nje gizani. Wazee hao wawili wamepangisha vijumba viwili vidogo. Kassech na mwanae wanaishi kwenye kijumba kimoja, Askale na Sam kwenye chumba kingine naye mlevi wetu Minabu anaishi kwenye kijumba cha tatu. Huyu mlevi angali akisikika akipiga kelele gizani.



## **SCENE FOUR: MIDNIGHT AT BELETU'S HOUSE**

### **52. SFX: NIGHT AMBIENCES AND THUNDER FROM OUTSIDE**

**53. Papa Tilahun:**     **(Whispers)** Hapana, hapa, usiwashe taa!

**54. Mama Beletu:**     Haya, Papa Tilahun, niache nijitazamie  
yanayotendeka nje. Mbona huyo mtoto amelia  
usiku wa manane?

**55. Papa Tilahun:**     Ebu ona! Tazama, Mama Beletu, Mpangaji  
wetu Kassech ...Anamkaribia... amemkamata.  
Nani huyo lakini? Ama ni mwizi?  
Ameshamkamata.

**56. Mama Beletu:**     Ebu nione, acha nitazame basi. Ni zamu  
yangu.

**57. Papa Tilahun:**     Hapana, subiri! Mwangalie nani huyo  
anayekuja! Anafanya nini huyu Minabu mlevi?

**58. Minabu:**           **(Outside from far)** Wewe hapo! Wewe, Amka  
Papa Tilahun, mzee mvivu wa kutupwa. Najua  
uko kitandani! Ha ha ha!

**59. Papa Tilahun:**     **(shocked)** Pengine ameshaniona?

**60. SFX:**               **TRAY FALLS DOWN**

**61. Papa Tilahun:** Nini hicho kilichoanguka? Ni nini hicho? Nini...

**62. Mama Beletu:** Ni sinia niliyoiegemeza mlangoni.

**63. Papa Tilahun:** Sinia?

**64. Mama Beletu:** Naam, sinia! Inaweza kukutahadharisha wakati wowote mwizi akituingilia. Sasa ni zamu yangu. Ebu nione e ...Oh! Hapa, anakuja huku tuliko.

**65. Papa Tilahun:** **(Frightened)** Nani...? Mama Beletu, usiseme kwamba mwizi anakuja kwetu.

**66. Mama Beletu:** Hapana, ni rafiki yako, Minabu mlevi.

**67. Papa Tilahun:** Zima taa mara moja!

**68. Mama Beletu:** Muda mfupi uliopita ulisema taa zisizimwe.

**69. Papa Tilahun:** Lakini sasa nataka kumfukuza mlevi huyu.

**70. SFX: WINDOW OPENS**

**71. Papa Tilahun:** **(Speaks through the window loudly)** Wewe! Nimeshakupata!

**72. Minabu:** **(Shouts frightened and runs away).**

**73. Papa Tilahun:** (laughs) Huyo anatimua mbio kama umeme. Alaa, naye mpangaji wetu mwingine anaelekea nyumbani mwake. Aha! Ameandamana na Jonas.

**74. Mama Beletu:** Jonas, ndugu yake mdogo?

**75. Papa Tilahun:** Naam! Nilidhani ni mwizi! Kesho asubuhi itanibidi kuzungumza na Kassech na pia huyo mlevi. Sasa, tulale.

**76. SFX:** **WINDOW CLOSED**

**77. SFX:** **WIND BLOWS OUTSIDE HARDER AND THUNDER**

**78. Narration:** Tuwaache Papa Tilahun na Mama Beletu walale. Hata hivyo huko nje, Kassech anarudi chumbani kwake akiandamana na Jonas, ndugu yake mdogo. Ana umri wa miaka kumi na mitano. Hajamakinika, na mara nyingine hulewa na pia kucheza kamari na vijana wenzake katika kitongoji hicho chao. Kassech amegundua kwamba mdogo wake huyo ana tatizo jingine.

### **SCENE FIVE: MIDNIGHT IN JONAS' PLACE**

**79. SFX: WIND BLOWS HARDER AND THUNDER**

**80. Kassech:** Hii ni laana! Bila shaka ni laana!

- 81. Jonas:** Ni sawa sasa! Nimeshazinduka!
- 82. Kassech:** Vyovyote vile! Hii ni laana! Mama yetu alifariki dunia kwa umaskini. Hatumjui baba yetu. Sasa na wewe umekuwa mtu wa kuota na kuweweseka usiku! **(She cries).**
- 83. Jonas:** Usinikemee katu! Mimi sitembei nikiota.
- 84. Kassech:** Usinihadae! Nateseka vya kutosha kuhangaikia riziki yetu ya kila siku. Ebu ikisie hatari inayokukabili kwa kuwa nje usiku!
- 85. Jonas:** Funga mdomo!
- 86. Kassech:** **(Surprised)** Ati! Mimi ni dadako mkubwa. **(In a low voice)** Sawa! Sasa usiku ni mpevu, twende ndani. Tutayazungumzia haya kesho asubuhi.
- 87. Jonas:** Usinisumbue na hiyo riziki yako! **(He walks away).**
- 88. SFX:** **STARTS TO RAIN**
- 89. Kassech:** **(Very shocked)** Ati? Rudi hapa! Mvua imeshaanza kunyesha. Rudi!
- 90. Jonas:** **(Laughs sarcastically)** Nitarudi nitakapozinduka usingizini... Mimi ninayeota nikitembea! **(He runs).**

**91. Kassech:** Mungu wangu! Unakwenda wapi? **(She cries).**

**92. SFX:** **RAINS HARDER**

**93. SFX:** **DOOR OPEND AND SLAMMED**

**94. Kassech:** **(cries frightened while she rushes inside)**

**OUTRO:**

Kwa kilio hicho cha Kassech tunahitimisha sehemu yetu ya kwanza ya kipindi chetu cha “ **Mwana Mpotevu- Kisa cha kina mama wawaleao watoto wao bila baba zao barani Afrika**”. Kwa nini Kassech akapiga kelele alipoingia chumbani mwake? Naye Jonas, mdogo wake Kassech, amekimbilia wapi usiku huo wenye mvua? Ili kufahamu hayo na mengineyo, jiunge nasi kwenye sehemu ya pili ya kipindi chetu. Kumbuka iwapo unataka kusikiliza kipindi hiki tena, au kuwasilisha maoni na mapendekezo yako, fungua ukurasa wa tovuti [dw.de/lbe](http://dw.de/lbe). Kwaheri kwa sasa!